



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WAKALA YA MABASI YAENDAYO HARAKA**



LAPF Tower, Ghorofa ya Pili, S. L. P. 724, Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 2700280/486 **Fax:** +255 22 2700603 **B-Pepe:** info@dart.go.tz **Tovuti:** www.dart.go.tz

Aprili 10, 2019

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **UPUNGUFU WA MABASI KATIKA MFUMO WA DART**

Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) inapenda kuujulisha umma kuwa leo, Jumatano, tarehe 10 Aprili 2019, kuna uhaba wa mabasi katika mfumo wa DART. Kupungua kwa idadi ya mabasi katika mfumo unatokana na baadhi ya mabasi kuwa na hitilafu na hivyo kulazimika kufanyiwa matengenezo makubwa na madogo.

Idadi ya mabasi inayotoa huduma leo katika mfumo wa DART ni 82 tu ambapo mabasi 58 yanafanyiwa matengenezo.

Kupungua kwa idadi ya mabasi waweza kusababisha usumbufu kwa wateja wetu.

Tunawaomba wateja wetu kuwa na subira wakati mabasi hayo yanafanyiwa matengenezo. Pia, tunawaomba radhi wateja wetu kwa usumbufu ambao utakuwa umejitokeza.

Aidha, tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu. Tunawashauri muendeleo kutufuatilia katika mitandao yetu ya kijamii ya Twitter (@DARTMwendokasi) na Facebook (DARTMwendokasi) kwa habari mpya za uboresha huduma zetu. DART ipo kwa ajili yako.

William V. Gatambi

**Meneja Uhusiano wa Umma**